

MAHITAJI YA JUMLA KWA MAOMBI YA CHETI CHA KIFO

- 1) kibali cha mazishi kutoka kituo cha tiba
- 2) Muhutajari wa kikao cha wanandugu wa marehemu kumteua msimamizi wa mirathi na barua ya utambulisho wa msimamizi wa mirathi kutoka kwa Afisa Mtendaji wa kata/kijiji ambapo tukio la kifo limetokea.
- 3) Kadi ya kupigia kura au kitambulisho cha utaifa wa marehemu.
- 4) Kitambulisho cha msimamizi wa mirathi na kinaweza kuwa kimoja wapo kati ha hivi; kadi ya mpiga kura, pasi ya kusafiria au kitambulisho cha utaifa.
- 5) Cheti cha ndoa au vyeti vya watoto vya kuzaliwa.

Mwombaji awe na nakala laini (soft copies) za viambatanisho vinavyotakiwa kuwa katika mfumo wa pdf kwa ajili ya kuviambatanisha baaada ya kukamilisha zoezi la kujaza taarifa katika mfumo nyaraka hizo ni kama zifuatavyo;

- ❖ kibali cha mazishi kutoka kituo cha tiba
- ❖ barua ya uthibitisho wa kifo kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kata
- ❖ Muhutajari wa kikao cha wanandugu wa marehemu kumteua msimamizi wa mirathi na barua ya utambulisho wa msimamizi wa mirathi kutoka kwa Afisa Mtendaji wa kata/kijiji ambapo tukio la kifo limetokea.
- ❖ Kadi ya kupigia kura au kitambulisho cha utaifa wa marehemu
- ❖ Kitambulisho cha msimamizi wa mirathi na kinaweza kuwa kimoja wapo kati ha hivi; kadi ya mpiga kura, pasi ya kusafiria au kitambulisho cha utaifa.
- ❖ Cheti cha ndoa au vyeti vya watoto vya kuzaliwa (kama mwombaji ni mke/mume au mtoto).

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- (i) Ada ya utoaji wa cheti kupitia mfumo kwa matukio ya vifo yaliyosajiliwa ndani ya muda Tshs 7000
- (ii) Ada ya usajili wa kifo kilichochelwa kuandikishwa ni Tsh 8,000 kwa tukio lililo chini ya miaka 10 na Tsh 20,000 kwa tukio zaidi ya miaka 10.

Mwombaji atatakiwa kuwa na nakala laini (soft copies) ya cheti chake cha kuzaliwa kinachotakiwa kuwa katika mfumo wa pdf kwa ajili ya kuambatanisha pamoja na viambata viwili kati ya vifuatavyo:

- a. kibali cha mazishi kutoka kituo cha tiba
- b. Muhutajari wa kikao cha wanandugu wa marehemu kumteua msimamizi wa mirathi na barua ya utambulisho wa msimamizi wa mirathi kutoka kwa Afisa Mtendaji wa kata/kijiji ambapo tukio la kifo limetokea.
- c. Kadi ya kupigia kura au kitambulisho cha utaifa wa marehemu.
- d. Kitambulisho cha msimamizi wa mirathi na kinaweza kuwa kimoja wapo kati ha hivi; kadi ya mpiga kura, pasi ya kusafiria au kitambulisho cha utaifa.
- e. Cheti cha ndoa au vyeti vya watoto vya kuzaliwa.

MAOMBI YA KUFANYA MAREKEBISHO KATIKA VYETI VYA VIFO

Huduma hii kwa sasa haipo kieletroniki na hivyo kuhitaji mwombaji kufika katika Ofisi zetu za Makao Makuu au Wilaya.

Marekebisho ya Jina la Marehemu

Marekebisho katika ya Sheria Usajili wa Vizazi na Vifo Sura ya 108 yaliyofanyika mwaka 2019, na kuruhusu marekebisho ya majina ya marehemu kama kuna herufi zimekosewa na sio kubadilisha jina lote au kuondoa majina ya marehemu.

Maombi hayo yatawasilishwa kwa barua kwa Msajili Mkuu na kuambatisha nyaraka za uthibitisho pamoja na kulipia ada iliyowekwa, na endapo maombi yatakidhi vigezo marekebisho hayo yatafanyika katika daftrari la usajili.

Angalizo; Jina linafanyiwa marekebisho na sio kufuta au kuondoa majina ya awali ya marehemu.

MAHITAJI YA JUMLA

- ◆ Barua ya kuomba marekebisho
- ◆ Cheti halisi kinachotakiwa kurekebishwa
- ◆ Viambata vinavyohibitisha marekebisho yanayohitajika mfano kadi ya kura au NIDA, vyeti vya shule, pasi ya kusafiria N.K
- ◆ Affidavit inaweza kuhitajika
- ◆ Ada ya malipo ya shilingi 13,000/=